CSDP
COTTON SECTOR DEVELOPMENT PROGRAMME

TANZANIA COTTON BOARD
TCB

# Matokeo ya kwanza kwenye majaribio ya Kilimo cha Mkataba ya Pamba katika kanda ya Magharibi 2016/17







Ripoti hii imeaadaliwa na
Board ya Pamba kushirikian na
Cotton Sector Development Programme (CSDP)

## Wigo wa Kilimo cha Mkataba Msimu wa kilimo 2016/17

Katika msimu wa kilimo 2016/17 mikoa ya Mara na Mwanza, inayowakilisha asilimia 18 ya ekari zote za pamba Kanda ya Pamba ya Magharibi, ilishiriki katika majaribio ya kilimo cha mkataba. Pia, baadhi ya maeneo ya uzalishaji mbegu na maeneo yenye utaratibu wa kilimo cha mkataba tangu zamani kati ya wachambuzi na wakulima wa pamba, walishiriki katika kilimo cha mkataba.[1]




Kwenye maeneo ya kilimo cha mkataba, wilaya iliidhinisha kupewa leseni kwa mchambuzi mmoja kununua pamba yote peke yake katika eneo alilopangiwa, lakini akitakiwa kuhudumia wakulima kwa kuwakopesha mbegu, viuadudu na huduma zingine.

## Mafanikio ya Kilimo cha Mkataba

Kwa mara ya kwanza katika miaka mitano, uzalishaji wa pamba haujashuka msimu huu. Kwa ujumla, uzalishaji kitaifa uliongezeka kwa 10%, kutoka tani 121,790 mwaka 2015/16 hadi tani 134,263 mwaka 2016/17. [2]

Maeneo ya kilimo cha mkataba yalichangia zaidi kwenye ongezeko hili la uzalishaji kitaifa kukiwa na ongezeko la asilimia 50.1 zaidi ya msimu uliopita ambapo maeneo ya nje ya kilimo cha mkataba yakiwa na ongezeko la asilimia 5.7.





Kipato cha mkulima kwenye maeneo ya kilimo cha mkataba kimeongezeka toka shilingi bilioni 12.6 msimu uliopita hadi bilioni 22.6 msimu huu, ikiwa ni ongezeko la 79%.

Thamani ya jumla ya uwekezaji wa wachambuzi katika maeneo ya kilimo cha mkataba ilikuwa shilingi 2.57 bilioni. 78.3% ya wakulima walipata mbegu kwa mkopo (ikiliinganishwa na 10.6% nje ya kilimo cha mkataba) na pia 72% wakipata viuadudu kwa mkopo (ikilinganishwa na 20.7 nje ya kilimo cha mkataba).
87.5% ya wakulima katika maeneo ya kilimo cha mkataba waliridhika au kuridhika sana na ufanisi wa upatikanaji na ubora wa pembejeo walizopata.

Kwa ujumla ubora wa pamba nyuzi ya Tanzania umeongezeka kutoka 21.7% daraja "GANY" au zaidi msimu uliopita, hadi 46% daraja "GANY" au zaidi msimu huu.[3]

## Eneo lililolimwa Pamba

Maeneo ya kilimo cha mkataba yalikuwa na ongezeko la eneo lililolimwa pamba kwa 33% kutoka ekari 113,102 msimu uliopita hadi ekari 150,058 msimu huu.




[1] Kwa ajili ya ripoti hii "maeneo ya kilimo cha mkataba" ni mikoa ya majaribio ya Mara na Mwanza tu.
[2] Bodi ya Pamba (chanzo pekee cha takwimu zote zilizotumika katika hii ripoti)
[3] Takwimu za usanifu pamba. GANY ni sawa na Kiwango cha ubora kimataifa "middling".


Ripoti hii imeaadaliwa na Board ya Pamba kushirikian na Cotton Sector Development Programme (CSDP).


Maeneo yasiyo na kilimo cha mkataba yalishuhudia kupungua kwa eneo lililolimwa pamba kwa 28%.

Pamba iliyoota ilikuwa pungufu ya pamba iliyopandwa kwa sababu ya ukame uliokuwepo msimu huu. Ongezeko la eneo limeonyesha nia ya wakulima kuendelea kulima pamba.

## Upatikanaji wa pembejeo: Mbegu za pamba

Mikoa ya Mwanza na Mara iliyokuwa na kilimo cha mkataba ilishuhudia ongezeko la matumizi ya mbegu kwa 177% na 74% msimu huu. Cha kushangaza mkoa wa Geita matumizi ya mbegu za pamba yalishuka kwa 61%.


Thamani ya mbegu zilizokopeshwa kwa wakulima msimu huu ilikuwa shilingi bilioni 1.27.











78.3% ya wakulima walipata mbegu kwa mkopo kwenye eneo la kilimo cha mkataba. Maeneo yasiyo na kilimo cha mkataba ni 10.6% tu ya wakulima walipata mbegu kwa mkopo.
91.2% ya wakulima katika maeneo ya kilimo cha mkataba waliridhishwa na upatikanaji na ubora wa mbegu walizopata.






## Upatikanaji wa pembejeo: Viuadudu

Mikoa ya Mwanza na Mara iliyokuwa na kilimo cha mkataba ilishuhudia ongezeko la matumizi ya viuadudu kwa 75% na 51% msimu huu. Vinginevyo, mkoa wa Geita matumizi ya viuadudu yalishuka kwa 70%.


Thamani ya viuadudu vilivyokopeshwa kwa wakulima msimu huu ilikuwa shilingi milioni 783.



Ripoti hii imeaadaliwa na Board ya Pamba kushirikian na Cotton Sector Development Programme (CSDP).



72% ya wakulima walipata viuadudu kwa mkopo kwenye eneo la kilimo cha mkataba. Maeneo yasiyo na kilimo cha mkataba ni 20.7% tu ya wakulima walipata viuadudu kwa mkopo.




82.7% ya wakulima katika maeneo ya kilimo cha mkataba waliridhika au kuridhika sana na ufanisi wa upatikanaji na ubora wa viuadudu walivyopata.



## Huduma za Ughani

Kulikuwa na maafisa ughani wa serikali na baadhi ya makampuni yaliajiri waghani wake. Lakini 28.8% tu ya wakulima katika eneo la kilimo cha mkataba walipata huduma za ughani, eneo lisilo na kilimo cha mkataba 20.8% tu walipata huduma za ughani.



## Ununuzi na bei ya pamba

Bei ya pamba ilikuwa shilingi 1,200/= kwa kilo katika maeneo yote na haikubadilika hadi mwisho wa msimu. Hakuna mchambuzi ambaye hakuwekeza kwenye kilimo cha mkataba aliyepewa leseni ya kununua pamba katika eneo la kilimo cha mkataba.

87.5% ya wakulima katika maeneo ya kilimo cha mkataba waliridhika na bei ya pamba iliyokuwepo.



## Uzalishaji wa Pamba

Jumla ya uzalishaji wa kitaifa iliongezeka kwa 10%, kutoka tani 121,790 msimu wa kilimo 2015/16 hadi tani 134,263 mwaka 2016/17.

Maeneo ya kilimo cha mkataba yalichangia zaidi kwenye ongezeko hili la uzalishaji kitaifa kukiwa na ongezeko la asilimia 50.1 zaidi ya msimu uliopita huku maeneo ya nje ya kilimo cha mkataba yakiwa na ongezeko la asilimia 5.7 kutoka tani 12,548 msimu uliopita hadi tani 18,834 msimu huu.

Mkoa wa Mwanza ulikuwa na ongezeko kubwa zaidi la uzalishaji kuliko mikoa yote Tanzania, toka tani 4,991 hadi tani 12,086. Hii ilikuwa ni ongezeko la 142%.

## Uzalishaji na kipato cha mkulima

Kipato cha mkulima kwenye maeneo ya kilimo cha mkataba kimeongezeka toka shilingi bilioni 12.6 msimu uliopita hadi bilioni 22.6 msimu huu, ongezeko la 79%[4]

[4]Jumla ya uzalishaji Mara na Mwanza msimu wa kilimo2015/16 ilikuwa kilo 12,548,353, kwa bei ya shilingi 1000 / kg. Jumla ya uzalishaji Mara na Mwanza msimu wa kilimo 2016/17 ni 18,833,973, kwa bei ya shilingi 1200 / kg.

Ripoti hii imeaadaliwa na Board ya Pamba kushirikian na Cotton Sector Development Programme (CSDP).